# AFRI TWENDE

Kulitia moyo kanisa la Afrika katika kazi ya umisheni ulimwenguni

Jarida la 8, Toleo la 2



# YALIYOMO











## 03 MCHUNGAJI NI UFUNGUO
Kiongozi wa umisheni na mchungaji, Ray Mensah, anatoa hoja za kwa nini wachungaji wanapaswa kuongoza makanisa yao kwenye umisheni.

## 04 TUMEITWA: MWENYE KASI KULIKO UPEPO
Toka uwanja wa mpira wa miguu hadi uwanja wa umisheni: mechi za kirafiki za kandanda nchini Angola zikawa kanisa la waumini 2000 ambalo linatuma watenda kazi wa Injili.

## 05 MCHUNGAJI: WAKILI WA UMISHENI
Mchungaji wa Nigeria, Azaki Nash anashirikisha mfano wake na ufahamu wa kuongoza kanisa la kimishenari.

## 06 MOYO WA MCHUNGAJI, ITIKIO LA KANISA
Mchungaji Meshack Rurangwa analitia moyo na kuliwezesha kanisa lake nchini Kenya kuvuka mipaka na Injili.

## 09 HAMASA NA RASIMALI KWA AJILI YA WACHUNGAJI
Tunashirikisha ushauri kutoka kwa wachungaji na wamishenari walioko mstari wa mbele na rasilimali ili kuwasaidia wachungaji kuhamasisha makanisa yao.

## 11 MBUZI NA VITUNGUU SWAUMU KWA AJILI YA INJILI
Wahamasishaji wa umisheni Sipho na Amanda Moyo wanatumia shamba lao nchini Zimbabwe kuandaa makanisa na watu binafsi kwa ajili ya umisheni.


© 2026 AFRITWENDE.

AFRITWENDE ni chapisho lenye lengo la kuinua ufahamu, hamasa, mafunzo na kuamsha makanisa na watu binafsi katika kuelekea kwenye huduma ya umisheni ulimwenguni.

**Mhariri Mkuu:** Samson Laurent

**Masanifu:** Pilgrim Communications

**Picha kwenye jalada**: Pastor Gordon Ansah (Anaconda Media)

Maoni yaliyoelezwa hapa katika makala mbalimbali katika Jarida hili si lazima yawe ya mchapishaji. Picha halisi hutumika mara chache. Majina ya bandia hutumika pale ambapo panahitajika kwa sababu za kiusalama.

*Jarida hili Haliuzwi bila kibali cha maandishi kutoka AfriTWENDE.*

www.afrigo.org/afritwende



# MCHUNGAJI NI UFUNGUO

## NA RAY MENSA MENSAH

Miaka michache iliyopita, kanisa moja lilinialika kuzungumza juu ya umisheni kwa siku mbili nyakati za usiku. Nilifurahi, lakini nilikuwa na hisia mchanganyiko. Ni watu wangapi wangejitokeza kwenye kongamano la umisheni siku ya Jumatano usiku? Kwa uzoefu wangu, washirika wachache wa kanisa huhudhuria programu kama hizo. Baada ya kufika, nilishtuka. Sehemu ya kuegesha magari ilikuwa imejaa, na mamia ya watu walijaza jengo hilo.

Askofu alisimulia jinsi ambavyo alijisikia hukumu kutoka kwa Bwana kwa sababu ya kuliacha agizo la kanisa, hata kusababisha hasara ya roho za watu kwenda kuzimu. Alianza kuhubiri juu ya uinjilisti, kufanya wanafunzi, na umisheni. Baada ya wiki kadhaa, alihisi walihitaji mtu aliye na uzoefu zaidi ili awawezeshe zaidi. Kwa hivyo, nilialikwa.

Niliondoka katika kanisa hilo nikiwa nimesadiki jambo nililokuwa nikisema—"MCHUNGAJI NI UFUNGUO!" Washirika wa kanisa hutenda kile ambacho mchungaji anasisitiza. Kwa maoni yangu, wachungaji wanahusika kwenye hali ya watu kutopenda umisheni tunayoiona katika makanisa Afrika na mabara mengine.

Dk. Michael Youssef anaiweka kwa njia hii: "Kama mimbari inavyoenenda, ndivyo na kusanyiko linavyoenenda. Kama kusanyiko linavyoenenda ndivyo na taifa linavyokwenda." Maandiko yanamwagiza kiongozi "awaandae watu wake kwa ajili ya kazi ya huduma, ili mwili wa Kristo ujengwe, hata sisi sote tufikie umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa watu wazima, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo" (Efe. 4:12-13). Kwa hiyo wachungaji lazima wajenge utamaduni huo wa kimishenari na kuwatayarisha washirika wa makanisa yao, kama jambo la dharura, kufanya wanafunzi na kupeleka Injili hadi miisho ya dunia.

Ingawa kwa sasa ninahudumu kama mkurugenzi wa shirika la kimisheni, kwa neema ya Mungu, nimechunga makanisa nchini Ghana, Botswana, na Namibia. Ninaelewa mashinikizo na changamoto zinazowakabili wachungaji; walakini, hicho sio kisingizio cha kuwa mtazamo wa kutazama ndani tu. Utume wetu ni wa kimataifa. Bwana wetu Yesu alituamuru, "Nendeni mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (Mt. 28:19-20).

Kwa muhtasari, wachungaji lazima wakamate maono ya uinjilishaji wa ulimwengu, kisha waingize maono hayo katika kusanyiko lao. Washirika wataitikia kwa kuchukua hatua katika Yerusalemu zao, Yudea, Samaria, na sehemu za mbali zaidi za ulimwengu. Kisha mchungaji anawaongoza kuunda sera ya umisheni ambayo itaathiri kila idara ya kanisa—watoto, vijana, wanawake, wanaume, kwaya, wahudumu, vyombo vya habari, n.k. Sasa umisheni unakuwa kiini kwa kila mtu anayehusika katika maombi, kutoa na kwenda. . Ninaomba hili lifanyike katika makanisa kote Afrika na kwingineko. Bwana wa Mavuno atumie toleo hili la AfriTWENDE kwa kusudi hilo.

*Ray Mensa Mensah ni Mkurugenzi Mtendaji wa OneWay Africa na pia anahudumu kama Rais wa Shirika la Wamishenari wa Kiinjili wa Ghana (GEMA). Ana shauku juu ya uhamasishaji kamili wa makanisa kwa ajili ya umisheni ambapo kila mshirika anahusika katika Agizo kuu. ray@owm.org.*

Vyanzo:

Lemons, J.D. The Pastor as the Missional Church Architect. Doctoral Thesis. Asbury Theological Seminary, 2007.

# NIMEITWA: DENILSON AGOSTINHO

## NENDA KWA KASI ZAIDI YA UPEPO

KAMA ILIVYOSIMULIWA KWA MERCY KAMBURA




Hebu fikiria kundi la vijana motomoto katika safari ya umisheni kwenda kwenye kundi la watu ambao hawajafikiwa kusini mwa Angola. Wanakaa kwa mwezi mmoja, wakihubiri, wakivunja vifungo, na kuwapatanisha wanakijiji na Muumba wao. Hatimaye, ni wakati wa kwenda nyumbani, lakini mavuno bado ni mengi. Mmishenari angefanya nini?

Nilikumbana na hali hii miaka mingi iliyopita. Kijana mmoja aliamua kwamba hatakuwa akifuatana nasi wakati wa kurudi nyumbani baada ya umisheni wa muda mfupi. Nilikuwa kiongozi wake, mwenye jukumu la kumrudisha yeye na wengine 14 kwa wazazi wao. Nikiwa na wasiwasi, niliripoti uamuzi wake kwa mama yake, nikitarajia kuadhibiwa. Lakini alisema, "Siwezi kupigana na Mungu. Ikiwa anataka kuwa mmishenari, na iwe hivyo."

Nikiwa kijana, tulicheza mechi na marafiki zetu. Siku moja, mtu fulani alipendekeza kwamba tusali mwisho wa mechi. Tulifurahia kusali pamoja sana mpaka ikawa tabia. Kila Jumapili, baada ya mchezo, tungekusanyika ili kuomba. Hivyo ndivyo nilivyookolewa.

Kikundi kidogo cha maombi kikawa kikundi cha kujifunza Biblia, na tulikuwa tukikutana mara tatu kwa juma. Miaka mitatu baadaye, kikundi hicho kikawa kanisa. Tulikua na washirika zaidi ya 100. Sote tulikuwa vijana bila uzoefu mwingi; kwa hivyo, tulimwalika kaka mmoja mwenye umri mkubwa kuliko sisi atuongoze na kuwa mchungaji wetu.

Kanisa hilo sasa lina umri wa miaka 15 na waumini zaidi ya 2000, wengi wao wakiwa vijana. Furaha yetu kuu sio idadi yetu, lakini kuhusika kwetu katika Agizo Kuu. Maneno ya kanisa letu, Born Again Church (Igreja Nascidos de Novo) huko Luanda, Angola, ni "huduma inayoleta matokeo katika mataifa."

Kila juma, tunahubiri mtaani. Kama wachungaji, tunaenda nao. Tunalifundisha kanisa kufanya uinjilisti kuwa mtindo wa maisha. Kila mtu anapaswa kuhubiri na kuwafanya watu watano hadi saba kuwa wanafunzi. Tulipanga ratiba na kueneza injili katika hospitali 16 tofauti.

Sasa ninatumika kama makamu wa rais wa kanisa. Mungu aliniita kuwa mmishenari baada ya safari yangu ya kwanza ya umisheni wa muda mfupi. Tunataka kanisa letu lihusike katika umisheni hadi uwe utamaduni wake. Makanisa mengi hayashiriki katika umisheni kwa sababu waumini hawajui jinsi ya kukutana na watu wapya na kuwashirikisha Injili.

### Kukuza kanisa la kimisheni

Uinjilisti sio kazi ya wikendi au likizo tu. Ni lazima ifanyike kila siku.

Kanisa barani Afrika linapaswa kwenda kwa kasi zaidi kuliko upepo ili kueneza Injili kwa waliofikiwa kwa uchache. Je, Kanisa linawezaje kufikia hili?

1. Usipoteze nafasi yoyote ya kuhubiri kila mahali.
2. Tumia nguvu, wakati, na shauku ya vijana na ufanye nao kazi.
3. Endesha mafunzo ya kila wiki ya jinsi ya kushirikisha Injili.
4. Kumbuka kwamba kiini cha Ukristo ni umisheni.

Yesu hakutuambia tukumbuke zaka na kadhalika. Akasema, "NENDA!" Mpendwa Mchungaji, usiruhusu kitu kingine chochote kuchukua nafasi ya maana ya Kanisa. Utume wa Kanisa ni kwenda. Ikiwa hutamwokoa jirani yako, je, unaelewa kweli kwa nini umeokolewa?

**TAFADHALI OMBA:**

- Kwa ajili ya rasilimali na fedha wakati tunaposafiri.
- Kwa ajili ya magari mazuri kwa ajili ya kwenda sehemu ngumu.
- Kwa ajili ya watenda kazi zaidi katika shamba la umisheni. Mavuno ni mengi.

# MCHUNGAJI:
## WAKILI MUHIMU WA UMISHENI

NA PASTOR AZAKI NASH

Kusudi la Mungu la ukombozi lililotimizwa katika Kristo Yesu na kuenezwa na mitume linabaki kuwa kazi ya Kanisa hadi Kristo atakaporudi. Wakati kanisa linapoelewa hili, kila kitu kinabadilika. Hapa ndipo penye jukumu la wachungaji kuhakikisha kwamba makanisa yao yamejikita katika umisheni.

Jukumu letu kama wachungaji hutupatia ushawishi wa kipekee katika kuelekeza kipaumbele cha kusanyiko kuelekea umisheni. Hii inatuhitaji kuwa na ari na mkakati wazi wa kutangaza umisheni wa ndani na nje ya nchi. Kusanyiko linapomwona mchungaji amekamatwa na mawazo haya, litafurika katika ushiriki wao katika kuwa kanisa linalofadhili umisheni na kutuma wamishenari.

Katika mwaka wa 2020, wakati wa janga la COVID, kanisa langu lilikuwa likifadhili wamishenari wa ndani 100 na wake zao wanaohudumu na Jumuiya ya Wamishenari ya Kiinjili (EMS) ya ECWA. Zaidi ya hayo, tulitoa msaada wa mara moja kwa mashirika na makanisa mengine ya kimishenari. Hili liliwezekana kwa sababu mchungaji ambaye alitangulia kabla yangu alikuwa na moyo wa umisheni.

Baada ya kushika nafasi kama mchungaji kiongozi mpya, niliazimia kuendeleza urithi huu kwa kuongeza ahadi yetu ya umisheni. Haikuwa vigumu kupata ushirikiano wa kusanyiko ili kuongeza kutoka wamishenari 100 hadi 125 mwaka wa 2021.

Mchungaji anapofikiri na kuzungumza umisheni, kusanyiko hujifunza kushiriki kikamilifu katika utume wa Mungu.

Jambo la msingi ni kwamba kanisa langu, ECWA Wuse II Abuja, Nigeria, liko kwenye umisheni kwa sababu wachungaji waliofuata waliweka msisitizo wa lazima kwenye umisheni. Mchungaji anapofikiri na kuzungumza umisheni, kusanyiko hujifunza kushiriki kikamilifu katika utume wa Mungu. Kila kanisa linapaswa kuwa na njia hii.

Lazima nisisitize kwamba uhamasishaji kwa ajili ya umisheni wa nje ya nchi unaweza kuwa mgumu ikilinganishwa na umisheni wa ndani. Ikiwa sarafu ya taifa italinganishwa na dola na kuwa na thamani ya chini sana, kile kinachoonekana kuwa ni kiasi kikubwa kitashuka thamani inapobadilishwa na kutumika katika nchi za kigeni. Suluhisho la busara ni kuongeza kiasi cha ufadhili, tuseme kwa kuzidisha mara dufu kile anachostahili mmishenari wa ndani. Hali hii inaonyesha kwamba wachungaji wanapaswa kufahamu wenyewe hadithi halisi za umishenari, mahitaji ya maombi, na changamoto.

Kama mawakili wa rasilimali za Mungu, wachungaji pia wanawajibika kutumia rasilimali kwa busara na usikivu wa kiroho mahali ambapo Roho Mtakatifu anaongoza (Efe. 1:17-18). Ni wajibu kwa wachungaji kuwa mawakili wazuri wa umisheni na wamishenari. Tunaweza kutumia kwa makusudi huduma zetu za ibada ya Jumapili ili kutoa taarifa za mara kwa mara za umisheni.

Kila mchungaji ambaye atakuwa na ufanisi katika kuhamasisha umisheni lazima aondoe maslahi binafsi, hata wakati ambapo timu ya uongozi inasitasita kutumia zaidi kwa ajili ya mmishenari kuliko kwa mchungaji wao.

Zaidi ya fedha, nyenzo na vitu, na rasilimali watu, kila shirika la kimishenari huthamini maombi ya watakatifu. Wachungaji wanapaswa kukusanya watu kuomba mara kwa mara kwa ajili ya umisheni.

Mimbari inatoa fursa ya kimkakati ya kutoa changamoto kwa washarika kuishi kimisheni kwa ajili ya Kristo. Wachungaji wanapohubiri Neno kwa uaminifu na kuwafundisha washirika kuwafikia waliopotea, kanisa litakuwa na waamini walio na nia ya utume. Huu umekuwa uzoefu wetu.

Kwa kumalizia, ninawaalika wachungaji wenzangu kujenga shauku ya umisheni, ili makanisa yetu yachochewe kwenda katika mataifa yote na Injili ya Yesu Kristo. Wito wetu kama wachungaji ni fursa ambayo tutaitolea hesabu atakapotokea Bwana wetu. Kwa hivyo, ninatoa wito kwa wachungaji wote kufanya kazi katika kujenga makusanyiko yenye afya na yenye kustawi ambayo yanapanua mipaka ya umisheni ndani na nje ya nchi—kwa ajili ya utukufu wa Kristo ambaye ametuingiza katika utume wake wa nyakati za mwisho (2 Wakor. 5:19-20).

*Azaki Nash ni mhudumu wa chuo kikuu, mwandishi hodari, mchungaji, na mmisiolojia. Mafunzo yake ya kihuduma*



*yanajumuisha Diploma ya baada ya kuhitimu ya Theolojia (PGDTh), shahada ya pili ya Divinity (MDiv), M.A. katika Uongozi na Usimamizi wa Shirika, na PhD katika Misiolojia. Yeye ni Mchungaji Kiongozi wa ECWA Wuse II Abuja, Nigeria. Ameoa na ana watoto wawili.*

www.afrigo.org/afritwende



Mafunzo ya uanafunzi katika kupanda kanisa jipya huko Goma, DR Congo

# MOYO WA MCHUNGAJI,
## ITIKIO LA KANISA

Baba yake alikuwa wa imani ya Kibaha'i na alifanya uuguzi. Alidai kuponya watu na kumtayarisha mtoto wake kufuata nyayo zake. Kwa bahati mbaya, hakuweza kujiokoa kutokana na ugonjwa uliomwua.

"Baada ya baba yangu kufa, niliona




uwezo wa juu zaidi kuliko ule wa baba yangu. Nilitamani kumjua Mungu, na mwaka wa 1998 nilitoa maisha yangu kwa Yesu na kubatizwa." Leo mwana huyo ni Mchungaji Rurangwa Muziga Meshack, ambaye anatumikia pamoja na waumini wake na wachungaji wenzake kupeleka Injili kwa kuvuka mipaka.

Mchungaji Meshack ni kiongozi wa umisheni katika Kanisa la Good Shepherd Church Nairobi, Kenya. Kanisa hilo ni sehemu ya madhehebu ya Kanisa la Africa Gospel Church linalofuata mizizi yake ya mwaka 1932 kazi iliyofanywa na wamishenari kutoka World Gospel Mission. Lilianza likiwa kikundi cha kujifunza Biblia, na baadaye likawa kanisa la kufikia jamii ya jirani. Mnufaika wa kanisa mwenyewe, Mchungaji Meshack alikuwa akihusika kama mhudumu anayepata mafunzo kazini (mazoezi) alipofika Kenya kama mkimbizi kutoka DR Congo. Hatimaye, alipewa leseni ya kuwa mhudumu wa wakati wote na akateuliwa kuwa mchungaji wa umisheni.

Kila kitu huinuka na kuanguka kwa kutegemea uongozi.

Umisheni ni shughuli kuu ya Kanisa la Good Shepherd Church. Kutoka makao yao makuu nchini Kenya, wameanzisha makanisa nchini Rwanda, Burundi, na mashariki mwa DR Congo. Kanisa lao linalofuata kuanzishwa liko Sudan Kusini. Kila kundi katika kanisa linahusika katika nyanja mbalimbali za umisheni—kuomba, kutoa kifedha, mafunzo, na kushiriki katika safari za kimishenari za ndani na za kimataifa.

"Kama John Maxwell alivyosema, 'mambo yote huinuka na kuanguka kwa kutegemea uongozi'", Mchungaji

Meshack anatushirikisha. "Mchungaji hushawishi kanisa kwa ajili ya umisheni kupitia uongozi wa mfano. Kama mchungaji, ninahubiri na kuwafunza kusanyiko kuwa waaminifu kutii Agizo Kuu. Pia ninahusika katika kwenda na kutoa. Umisheni hauwezi kufanywa na mchungaji peke yake; washirika lazima pia waombe, watoe, na waitie moyo timu ya wachungaji."

Hakuna kinachofanyika nje ya mpango wa kanisa, na lengo la utume la Good Shepherd limekita mizizi katika mikakati yao muhimu: kuinjilisha ambao hawajaokoka, kuanzisha makanisa, kuwajenga waumini, kuandaa viongozi, na kuonesha huruma. "Umisheni sio tu idara ya kanisa au shughuli; ndiyo sababu ya kanisa kuwepo, kwa hiyo tumejitoa kufanya hivyo," Mchungaji Meshack anasema.

## Maombi na mafunzo

Kila kitu huanza na maombi. Kanisa hukutana kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi ili kuombea kila wanachofanya, ikiwa ni pamoja na umisheni. Timu yao ya maombezi pia hukutana Jumamosi kwa kusudi hilo. Wanaomba msaada wa Mungu kumtambua mtu anayefaa kumtuma kwenye umisheni, na kuwaonyesha ni nchi gani au eneo gani la kwenda. Wanachangisha pesa kwa maombi, wakimwomba Mungu awatume watoaji na kuwafanya watu wawe tayari kuunga mkono.

Kila mwaka, Oktoba ni mwezi maalum wa umisheni. Kanisa huwaalika watu kuzungumza juu ya mada maalum kuhusu umisheni na kuwahimiza washirika kutoa kwa ajili ya wamishenari na kwenda umisheni. Wanawafunza washirika kuwa na mtazamo wa Agizo kuu na kushirikisha Injili kwa njia ya urafiki, kutoa kwa wale wanaohitaji, na kuwaombea wanaoteseka.

Mchungaji Meshack anatushirikisha hadithi ya John: "Wakati kanisa lilipofanya mafunzo kuhusu kufanya wanafunzi kwa ufanisi, John alihudhuria na baadaye akapata nafasi ya mafunzo katika benki. Alianzisha wazo la kujifunza Biblia na vipindi vya maombi kila siku kabla ya kazi. Alipewa ruhusa, na kila mtu akapenda kujiunga. Wenzake wengi waliorudi nyuma walianza tena kusoma Biblia zao na kuhudhuria kanisa. Leo, wamepata chumba cha kukutana kwa ajili ya sala, ibada, na kujifunza Biblia. John alikuwa amechochewa na kile ambacho kanisa lilikuwa likifanya. Lengo letu ni kuwasaidia washirika wa kanisa kufuata hatua za Yesu kwa kuwafundisha kufanya wanafunzi."



Washiriki wa timu wakikabiliana na ukweli kwamba hili litakuwa kanisa lao wakati wa safari yao ya umisheni.

## Uhamasishaji na uandaaji

Kanisa huwaandaa washirika walio tayari kuitikia wito wa Mungu na kuhudumu katika umisheni. Wanawafundisha kuhusu utamaduni wa watu, kanuni za mavazi na imani zao, na jinsi ya kuwasiliana. Kanisa hupanga safari za umisheni za muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi, na washirika hujiandikisha kwenda wenyewe au kusaidia wale ambao wanataka kwenda lakini hawana pesa. Safari za kimataifa hufanywa kila robo mwaka au kulingana na mpango wao wa kanisa kwa mwaka. Wana bajeti ya kila mwaka ya umisheni na pia kutenga sehemu ya matoleo yao ya kawaida kwa madhumuni hayo. Kanisa lina maeneo matatu ya umisheni na wamishenari ambao wanawasaidia kifedha na kwa kuwatembelea mara kwa mara.

> Mungu anapokuita katika huduma, Yeye huenda pamoja nawe na kukusaidia.

## Hamasa ya Mchungaji

Kwa kusanyiko la watu 600 hivi, kufanya umisheni si rahisi. "Changamoto kubwa imekuwa fedha. Tunaendesha huduma zetu zote bila kutegemea msaada kutoka nje. Ubaya mwingine ni kwamba kusanyiko kwa sehemu kubwa ni la wahamiaji ambao huendelea kuhama. Ni vigumu kuwa na wafanyakazi wa kujitolea wa kudumu na washirika ambao wanaweza kushiriki kikamilifu katika kazi ya kanisa. Vikwazo hivi hutufanya tushindwe kutuma wamishenari zaidi, ingawa tungependa kufanya hivyo."

Hata hivyo, anatoa ushauri na kutia-moyo: "Mungu anapokuita katika huduma, Yeye huenda pamoja nawe na kukusaidia. Hii imeniongoza kumwamini Mungu, lakini yeyote anayetaka kuitikia wito wa umisheni wa Mungu lazima awe tayari kwa shida na furaha. Mtu hata hivyo hapaswi kuogopa au kutilia shaka mambo yanapokuwa magumu—hiyo ni sehemu ya wito wetu katika umisheni. Nimejifunza kutumia rasilimali zilizopo kufanya kile ninachoweza kwa wakati huo, badala ya kutofanya chochote. Huduma yetu inafanya kazi kwa imani; si kwamba tunaweza kujikimu, bali Mungu hutupatia mahitaji yetu kwa njia yake mwenyewe.

"Ili kanisa lijihusishe sana na umisheni, ni lazima lianzie kutoka moyoni mwa mchungaji. Wakati fulani kanisa linaweza kuhusika katika mambo mengi na kupoteza moyo wa umisheni. Mchungaji anapojua sababu ya kuwepo kwa Kanisa, umisheni utakuwa kipaumbele chake."

# KULIFANYA KANISA LAKO LIWE LA KIMISHENI

## KUMWEZESHA MSHIRIKA WAKO KUINGIA KATIKA UMISHENI

Na Mchungaji Faith Mugera, Mchungaji wa Ushirikiano wa Kimataifa na Umisheni, Nairobi Chapel

Nairobi Chapel ni kanisa kubwa lenye nia ya umisheni nchini Kenya. Wametuma wamishenari 31 na timu 33 za muda mfupi na wana matokeo katika nchi 16. Faith Mugera, mchungaji wa umisheni, anashirikisha mawazo sita ambayo wameanzisha ili kuratibu programu yao ya umisheni.

1. **Thibitisha wito wao**
   Jua safari iliyopelekea uamuzi wao. Washirika wetu hawaendi peke yao, kwa hivyo tunataka kuelewa jinsi tunavyoweza kuthibitisha na kuhusika na wito wao.
2. **Ujenzi wa tabia**
   Tunawasilisha mafunzo ya uanafunzi na tunasihi ili kuwatayarisha na kuwategemeza katika wakati wao wakiwa mbali. Ni muhimu kwamba hii iendelee kwenye eneo watakaloenda.
3. **Mafunzo ya utamaduni**
   Kuanzia na mawazo ya kimsingi kuhusu utamaduni, tunataka wazamishwe, wavunje fikra potofu, wasikilize vyema, wawe sehemu na wajenge mahusiano yanayodumu.
4. **Kujidhatiti/Kujitoa kwa dhati kwa ajili ya wito**
   Tunawaomba washiriki wetu waweke viapo vya utauwa, usafi, na umaskini, au karibu na hizi kama ilivyokubaliwa.
5. **Kuwaagiza**
   Tunamsherehekea na kumtuma mmishenari hadharani. Kwa kawaida tunafunza vikundi vyao vidogo kuendelea kuwaunga mkono kwa kuwatembelea, kupiga simu, na kutuma vifurushi vya zawadi.
6. **Kanisa**
   Daima tunashirikiana na kanisa la nyumbani. Wanashughulikia visa, bima, na malazi. Tunawategemeza wamishenari wetu kifedha, kwa hiyo hawajahitaji kutafuta ufadhili.

## KUELEKEA MAKANISA YENYE NIA YA UMISHENI ZAIDI

Ndivhuho Ranwedzi, Mchungaji Kiongozi, The Apostolic Faith Mission of South Africa Revival Centre, Atteridgeville

Agizo moja ambalo kanisa linapaswa kukumbuka ni Mt. 28:19: "Kwa hiyo enendeni mkafanye wanafunzi kutoka katika mataifa yote, mkiwabatiza katika jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu."

Kanisa linaloenda haliko kwenye jengo lake tu, bali linajali kuhusu mazingira yake ya mahali lilipo na kiulimwengu. Je, unaweza kufikiria kanisa ambalo shauku yake pekee ni kuona watu wakimiminika katika jengo lake siku za Jumapili? Hakika, kanisa hilo litajitenga na uhalisia wa jamii yake na upesi halitakuwa na maana.

Ni muhimu kwa mchungaji kutafakari juu ya mwitikio wa kanisa juu ya changamoto za kijamii ndani ya jumuiya yake na kwingineko. Mbinu itabidi iwe ya kimkakati wa kimisheni wa makusudi unaoounganisha kanisa na jamii. Kanisa halipaswi tu kuwa la kuvutia katika njia zake, bali pia la kimishenari. Kanisa la kivutio pekee hukosa fursa ya kuathiri ulimwengu. Wachungaji ni muhimu katika kuelekeza kanisa kwenye umisheni, na njia moja wanayoweza kufanya hivyo ni kwa kutoa programu za kujenga uwezo.

Juhudi za kimishenari zimetumiwa zaidi na madhehebu kongwe ya Kikatoliki na Kiprotestanti kuliko makanisa ya hivi karibuni ya huduma huru. Hata hivyo, nyingi za huduma hizi zinazojitegemea zina rasilimali za kutosha kutekeleza kazi hiyo na kuleta matokeo makubwa. Kwa kawaida, nao huanza na ladha ya kimishenari lakini hufikia hatua ya kuvutia, hasa wanapojulikana sana. Ninawahimiza wachungaji wa makanisa kuungana tena na Mt. 28:19.



PICHA NA AIM STORIES




# MCHUNGAJI WETU ALIFANYA WITO WETU WA KIMISHENARI UWEZEKANE

Na Patrick Nabwera

Maombi yamekuwa hitaji muhimu sana. Mke wangu na mimi hutumika mbali na nchi yetu, na mchungaji wetu huko nyumbani huhamasisha kusanyiko lote kutuombea. Angewaambia kwenye ibada ya Jumapili waangalie upande wa eneo letu la umisheni na kuomba, kisha anahitimisha maombi.

Wakati mmoja, mchungaji wetu hakuweza kutusaidia kifedha. Alinishika mkono na kuomba, "Mungu, hatuna cha kuwapa, lakini tunaomba kwamba uwafadhili." Na kwa hakika, Bwana alitufadhili. Mchungaji wangu alikuwa mwaminifu, na nilijua hali hiyo. Wakati ulipofika, alihamasisha kanisa kutusaidia kwa rasilimali.

Wakati mwingine, alimtuma dada kututembelea katika eneo letu la umisheni, umbali wa kilomita 2500 kwa barabara. Kumuona dada huyu ilikua kama kumuona malaika. Uwepo wake haukuwa wa kutia moyo tu, bali pia fursa kwake ya kurudi na kumshirikisha mchungaji na kanisa uhalisia katika eneo letu la umisheni. Hii iliongeza maombi na hali yao kutujali.

Watoto wetu walikuwa katika shule si mbali na kanisa letu la nyumbani na mara nyingi, hatukuweza kuwatembelea kwa sababu ya umbali. Mchungaji wetu, mke wake, msaidizi wake, na baadhi ya washirika wa kanisa walikuwa wakiwatembelea. Msaada huu ulitufanya kujua hatuko peke yetu.

Wakati wa mapumziko yetu nyumbani, mchungaji wetu alitualika kushirikisha shuhuda zetu na kusanyiko. Baadaye, alijiunga na kikundi kidogo kilichokuja kusikiliza hadithi zaidi. Uwepo wake katika mkutano ulifanya wengine waone umuhimu wake. Kando na hili, kila mara alitengeneza muda wa kushirikiana, kusikiliza safari yetu ya umishenari, na hatua zinazofuata. Aliwakumbusha daima kusanyiko kututegemeza, na hilo likaongeza thamani ya kazi yetu machoni pa kanisa letu.

Ninalinganisha umisheni wa kwenda tamaduni tofauti na kutembea kwa miguu miwili. Mguu mmoja ni "unaenda" na mwingine "unatuma." Kama vile inavyochosha, ni wa polepole na inachosha kuruka kwa mguu mmoja, ndivyo ilivyo kwa kufanya umisheni kwa mguu mmoja - kwenda bila kutuma. Paulo anauliza, "Na watawezaje kuhubiri isipokuwa wametumwa?" (Rum. 10:15a) Na Yohana anasema wale wanaotuma wanapaswa kutuma kwa namna impasayo Mungu (3 Yoh. 6).Na ufunguo wa kanisa la mahali ni kiongozi wake, mchungaji.

# WAJIBU WA MCHUNGAJI KUAMSHA MOYO WA UMISHENI KATIKA KANISA LA TANZANIA

## NA MWINJ. JOEL NKANDA SIMBITTI

Mimi nilizaliwa na kumwamini Yesu kwenye moja ya makanisa ya Kiinjili Tanzania (evangelicals). Chakushangaza ni kwamba nilijua kuwa umisheni ni kazi ya mzungu (white man's work)! Nilipojiunga na chuo cha theologia, Scott Christian University, mwaka 1994 nilifumbuliwa macho. Mwalimu wangu, Dkt. Richard Gehman, alianza kukaribisha wamishenari wazalendo kwenye ibada za wanafunzi (chapel) kuja kutoa shuhuda zao. Nilishtuka sana wamisionari Wakenya wakitambulishwa kwenye ibada zetu! Mimi nilitarajia sana kumwona mmisionari kutoka nchi za Magharibi. Hata hivyo shuhuda za wamisionari hao ziliugusa sana moyo wangu mpaka nilianza kulia machozi. Moyoni nilijisikia deni kubwa kwa ajili ya makabila mengi bila Injili ya Kristo Tanzania!

Matokeo yake niliyatoa maisha yangu kwa ajili ya umisheni na kupanda makanisa. Nilifundisha na kuhamasisha watu binafsi, makanisa, vikundi makanisani na vyuo vya Biblia/Theologia kufanya umisheni. Kwa uzoefu huo nikaelewa wajibu wa mchungaji kulifanya kanisa kuwa la kimisheni. Kwa mfano mwaka 2000 nilipeleka wanafunzi 2 kutoka chuo cha Biblia kwenda mafunzo kazini kwa Warangi mkoani Dodoma. Wanafunzi hao walifanya kazi na mmisionari mzalendo Peter Pharles Kisenna. Miaka 20 baada ya umisheni, Kisenna alianza kuchunga kanisa na alilolihamasisha kufanya umisheni. Baada ya kuongoza kanisa, Kisenna alikwenda kufundisha vyuo vya Biblia, na akiwa huko aliunda huduma ijulikanayo kama Triple Mission for Christ (TMC). TMC iliwaunganisha wanafunzi wa vyuo na wakristo makanisani kuunda timu ya kuyafikia makabila yasiyofikiwa. Mwaka 2022 Kisenna alichaguliwa kuwa Askofu kwenye dhehebu lake, kwa nafasi yake anawaongoza Wakristo kwenda kuwafikia Wataturu, Warangi na Wamasai katika mikoa mbalimbali nchini Tanzania.

Pia nimejifunza wajibu wa mchungaji katika huduma ya umisheni kupitia kuyahamasisha makundi ya kwaya za kufanya umisheni. Mwaka wa 2020 niliitwa na kwaya ya Vijana Geita kuwafundisha jinsi ya kufanya umisheni. Mwanzoni, mchungaji wao John Masanyiwa, hakuhamasika sana lakini baada ya kupokea maono, mchungaji huyo ndiye mbeba maono ya umisheni katika kanisa la Africa Inland Church Tanzania. Mpaka sasa Masanyiwa ameliongoza kanisa lake kuyafikia makabila ya Wanyambo, Wasonjo, Wamasai na Wabarabaig (Wamang'ati).

Mchungaji mwingine ni Samwel Lupilya aliyestaafu miaka 3 iliyopita. Lupilya alikuwa mmisionari kwa Wabarabaig kabla ya kwenda kuchunga makanisa. Hivyo alichunga makanisa ya Malya, Makongoro na Buzuruga na katika makanisa yote Lupilya aliwahamasisha Wakristo kuwafadhili, kuwasomesha na kuwategemeza wamisionari shambani. Kwa nia hiyo mchungaji huongoza timu kutoka makanisani kwenda kufanya umisheni na kupanda makanisa ndani na nje ya nchi. Kwa mfano ameongoza timu za kupanda makanisa kwa Wataturu licha ya safari za kimisheni kwenda Kongo (DRC) na Msumbiji.

Tukitaka kanisa la Kristo duniani liutii Utume Mkuu lazima wachungaji wabebe maono ya umisheni. Mchungaji akitaka kanisa lake liwe la kimisheni lazima afanye yafuatayo: (a) afundishe na kuhubiri umisheni (b) awakaribishe wamishenari kanisani (c) aliongoze kanisa lake kwenye safari za kimisheni (d) alipeleke kanisa kwenye safari za kimafunzo kwenye makanisa yanayofanya umisheni.



*Mwinj. Joel N. Simbitti, Mkurugenzi wa Huduma za Kiroho AICT na Mratibu wa Mtandao wa Umisheni Tanzania.*

### Fahamu zaidi kuhusu AfriTWENDE!

Kwenye tovuti yetu, tuna matoleo matano ya Kiswahili! Kila toleo lina makala ambayo itakufundisha zaidi kuhusu umisheni, kukuarifu kuhusu kile wamisionari wanafanya shambani, na kukuchochea kuwa hodari katika imani yako. Unaweza kuona makala yote na kupakua masuala bila malipo kwenye tovuti yetu kwa www.afrigo.org/afritwende.

# MBUZI NA VITUNGUU SAUMU KWA AJILI YA INJILI

## KAMA ILIVYOSIMULIWA KWA KATE AZUMAH

"Purple Horizon ndio jina la shamba letu. 'Zambarau' hurejelea mti maalum unaogeuka zambarau kila Oktoba na umuhimu wake kama mahali pa sala. Pia inawakilisha ukuu wa Bwana Yesu. 'Horizon' inarejelea uwezekano usio na kikomo kwa Waafrika wanaojihusisha na Umisheni na mamilioni ya watu wanaongoja Injili. Tunaona shamba kama mahali pa kulitayarisha Kanisa kwa ajili ya umisheni wa kuvuka tamaduni, kuandaa wahudumu wa umisheni binafsi, na kutengeneza njia za fursa za Injili."

Sipho na Amanda Moyo wamekuwa wakifanya kilimo na uhamasishaji na ACTS13/WEC International kwa miaka saba. Wanafurahia ndoa ya tamaduni tofauti na wanaishi katika mji wa Sipho wa Kwekwe, Zimbabwe. Kanisa lao la nyumbani ni Kwekwe Central Baptist, na Muungano wa Wabaptisti wa Zimbabwe unawatambua kama viongozi wa umisheni. Pia wanafundisha kuuelewa umisheni kwa watu wa Assemblies of God. Sipho ni mchungaji, na timu yao ya uhamasishaji imeundwa na marafiki wachungaji. "Wachungaji wanaoungana na wachungaji hufungua milango makanisani kwa sababu kazi ya wamishenari ni ngeni kidogo," akina Moyo wanasema.

> Wachungaji wanaoungana na wachungaji hufungua milango makanisani kwa sababu kazi ya wamishenari ni ngeni kidogo.

### Vitunguu saumu, mbuzi, na zaidi

Akina Moyo wanakili jaribu la kutaka kulima kila kitu; hata hivyo, Bwana aliwaongoza kulima vitunguu saumu na kufuga mbuzi kama viwanda vyao vya msingi. Kitunguu saumu ni zao maalum na lina uwezo mkubwa wa kutengeneza pesa. Ili kuiweka huru dhidi ya wadudu na magonjwa, huizungusha kwa kupanda mimea mingine kama karanga na maharagwe ya sukari. Pia wanalima mahindi, mtama, alizeti na karanga. Wana mradi mdogo wa kuku na ufugaji wa samaki karibu.

Amanda anaeleza, "1 Thes. 4:11-12 imetuchochea kuishi maisha ya utulivu na kufanya kazi kwa mikono yetu ili tuenende ipasavyo kwa wale walio nje na tusipungukiwe na kitu. Tunaamini shamba siku moja litatutunza sisi na wahudumu wengine wa Injili wanaokwenda nje ya Zimbabwe. Kwa sasa, tunatumia fursa zilizopo ili kufanya shamba letu kumtumikia Mungu katika umisheni."

Wametoa mafunzo kwa watenda kazi wanaokwenda na ujuzi wa kilimo, ambao nao wameanzisha maeneo kama hayo katika vituo vyao vya umisheni nchini Kenya na Nigeria. Wachungaji wengi wametembelea na kupokea maono makubwa zaidi ya umisheni. Watenda kazi wanaokuja kupata mafunzo huja kwa ajili ya maendeleo ya umisheni na akina Moyo hutoa maono ya kufanya kazi kwa bidii kwa mikono ya mtu mwenyewe kwa utukufu wa Mungu.

"Mara nyingi, tunauza ndani au kutoa msaada kwa jamii yetu kuungana nao na kujenga mahusiano." Kituo cha msaada wa makanisa, familia, na marafiki husaidia katika kazi.

"Vitunguu saumu vyetu vilienda vizuri mwaka huu. Tulitarajia kusaidia wamishenari kwa faida, lakini soko limekuwa dhaifu. Inavunja moyo kushikilia zao hilo la thamani; lakini tunasonga mbele, kwa kuwa Bwana alitupa mwongozo." Wana Moyo wanashauri:

- Ombea maisha yako, kile ulicho nacho mkononi mwako na mazingira yako. Anzia hapo ulipo.
- Kuwa na wazo la biashara na uandike mpango wa kina. Unaweza kubadilika mara 100. Umisheni unahusu kuwaleta wengine pamoja, na wakiona mpango wako kwenye karatasi, wanaweza kukuamini.
- Mtumaini Mungu. Mipango inaweza kushindwa, lakini Mungu hafanyi hivyo. Kupata faida inachukua muda. Tumikia na Toa na Penda.
- Ona masomo ambayo Mungu atakufundisha. Yatakusaidia kupata hekima na uzoefu.

Sipho na Amanda Moyo
moyosinzim@gmail.com





# KUNDI LA WATU: WABAKA

Watu wa kabila la Wabaka wa kusini-mashariki mwa KamerunI ndio kundi kubwa zaidi kati la Mbilikimo kadhaa waliotawanyika kote Afrika ya Kati. Mbilikimo wana kimo kidogo, likiwa na wanaume watu wazima wasiozidi sentimita 155.

Wabaka wanaabudu roho ya msitu iitwayo Jengi (pia inajulikana kama Djengui au Ejengi). Wengi wanaishi katika kambi ndogo au vijiji vilivyotawanyika katika misitu ya bonde la Mto Kongo. Wao huwa wawindaji-wakusanyaji, kukusanya chakula chao cha kila siku kutoka kwa wanyama na mimea katika msitu wa mvua. Miti inapovunwa na wanyama kusumbuliwa, hali inazidi kuwa ngumu zaidi kutunza familia zao. Wengine wameanza kupanda mashamba na kufanya kazi kwa makabila jirani ya wakulima, lakini malipo ni kidogo.

Wabaka wanaona umaskini wao na kudharauliwa na wengine kama ushahidi wa uduni wao. Makabila mengine yanawapa hadhi ya chini kutokana na kimo na mtindo wao wa maisha. Walakini, wanaheshimu "kiroho" chao na uhusiano wao na uumbaji, wanakuja kwao kwa ajili ya kupata dawa.

Baadhi ya wamishenari kutoka World Team wamekuwa miongoni mwa Wabaka kwa zaidi ya miaka 16, wakijifunza lugha yao na kufanya uinjilisti na uanafunzi. Wanatoa mafunzo kwa wachungaji na viongozi, wakiwatia moyo kutumia utamaduni na ujuzi wao kufanya maisha bora na kanisa lenye nguvu zaidi kwa watu wao. Viongozi wachache wa makanisa mara nyingi hufanya kazi kwa wakulima wa jirani, zikiwaondoa kwenye kazi zao za kanisa.

Maisha yao ya kuhamahama na maeneo ya mbali hufanya elimu rasmi kuwa ngumu. Wabaka wengi hutumia njia za masimulizi kurithisha mila na desturi zao. Shirika la kimisheni, SIL, limeunda seti ya hadithi 37 za Biblia kwa ajili ya uinjilisti na mafundisho.

Ingawa kuna makanisa madogo yanayokua, kambi nyingi na vijiji havina ushuhuda wa Injili wenye nguvu. John Paul Gouffo, Mkameruni na Christian Missionary Fellowship International (CMFI), ni mmoja wa wamisionari wa kwanza wa ndani kwa Wabaka.

## Kwa Kifupi

- Wabaka wanaamini katika Mungu muumbaji, Komba, lakini wanamwona kuwa yuko mbali. Badala yake wanamfuata na kumwamini Jengi, roho wa msituni.
- Uwindaji na uvuvi ni muhimu kwa utamaduni wa Baka, nao huweka vijito vya maji ili kuvua samaki.
- Wabaka wengi wametingwa na shughuli nyingi sana kila siku za kuwasaidia kuishi maisha yao hata wasiweze kufikiria mambo ya kiroho.

## Omba kwa ajili ya

- Kazi inayozaa matunda ya watafsiri wanaojifunza lugha ya Wabaka na kuitafsiri Biblia kwa lugha hiyo.
- Bwana kujibu maombi ya Wakristo wa kabila la Wabaka ili kujenga imani yao.
- Umoja na baraka kati ya makanisa na huduma mbalimbali zinazohusika na Wabaka, na kwa waumini wa Wabaka kufikia watu wao wenyewe.

Vyanzo: Wikipedia na wamishenari wa World Team


SIM By Prayer
AFRICA INLAND MISSION

**AFRITWENDE**: afritwende@afrigo.org **AFRIGO**: info@afrigo.org **ALLONS-Y !** : info@afrigo.org **AFRÍDE**: afride@afrigo.org

**SIM Afrika Mashariki**
**Sm:** +251 911 206 530
east-africa.office@sim.org

**SIM Afrika Magharibi**
Sm: +233 30 222 5225
wamo.personnel@sim.org

**SIM Kusini mwa Afrika**
Tel: +27 21 7153200
za.enquiries@sim.org

**AIM Kimataifa**
amc.io@aimint.org
aimint.org/africanmobilization/